

## UMOJA WA KIMATAIFA WA WANASAYANSI YA JIOLOJIA

Sayansi ya Ardhi Ulimwenguni

Nini maana ya IUGS?

Umoja wa Kimataifa wa wanasayansi ya jiolojia ulioanzishwa mwaka 1961 ni moja ya asasi kubwa sana duniani.

Umoja huu unahamasisha ushirikiano wa kimataifa na ushiriki katika sayansi ya ardhi kuhusiana na manufaa ya binadam na umoja huu ni mwanachama wa Kanseli ya Kimataifa ya Sayansi.

Uanachama uko wazi kwa nchi au maeneo yalioainishwa.

IUGS ina nchi wanachama zaidi ya 100 wanawakilisha zaidi ya wajiosayansi milioni moja

IUGS inafanyakazi kwa kuzingatia Tume za mada maalum, vikosi kazi, na ubunifu na program za pamoja kati yake na asasi zingine.

Kwa sasa inatengenezwa na:

Tume:

- Elimu ya Jiosayansi, ufundishaji na kurithisha teknolojia.
- Jiosayansi kwa ajili ya Mipango ya Mazingira
- Historia ya Sayansi ya Jiolojia
- Menejimenti na Matumizi ya Taarifa za Jiosayansi
- Stratigrafia
- Mitetemo na jiolojia ya miundo ya miamba

Program za pamoja:

- Program za kimataifa za lithosfia
- Matumizi ya Jiolojia katika "Remote sensing"
- Isotopi na jiokronolojia
- Ushiriki wa kimataifa wa kijiosayansi (tazama chini):
- Mikutano ya kimataifa ya kijiolojia (tazama chini):

Vikosi kazi:

- Misingi ya jiokemia duniani
- Nguvu kazi ya jiosayansi duniani
- Mawe ya urithi
- Urithi wa kiolojia
- Taaluma ya jiosayansi duniani

Mpango:

- Forensic geology (IFG)
- Rasilimali kwa vizazi vijavyo (RFG)

Taarifa zaidi zinaweza kupatikana katika website ya IUGS [www.iugs.org](http://www.iugs.org)

Ushirikiano wa Kimatifa wa Jiosayansi wa IUGS/UNESCO

Tangu mwaka 1972, program hii ya flagship inayofadhiliwa kwa pamoja kati ya IUGS na UNESCO, imefadhili wajiosayansi wenye changamoto za kiuchumi na kisiasa kuweza kushiriki tafiti na miradi ya kimataifa.

Mkutano wa Kimataifa wa Kijiolojia (IGC)

Kwa mara ya kwanza ulifanyika 1878. Mkutano huu wa kila baada ya miaka minne, ndiyo tukio kuu sana kwa sasa katika kalenda ya sayansi zote za arthi. IUGS imekuwa ikijihusisha katika uongozi tokea mwaka 1961 lakini kwa sasa IUGS inahusika pia katika Mikutano. Mkutano wa aina hii unaofuata utafanyika Cape Town Afrika Kusini mnamo mwaka 2016 na maelezo yake yanapatikana katika website ya IUGS.

Episodes (Matukio)

Jarida la IUGS linalotoka mara nne kwa mwaka linatoa taarifa za maendeleo ya jiosayansi yenye umuhimu kikanda na kimataifa. Pia linatoa majarida ya kitafiti asilia. Mambo mbalimbali ya sasa na yaliyopita, yanapatikana bure katika [www.episodes.co.in](http://www.episodes.co.in) au katika website ya IUGS.

Jarida hili linaloandikwa kwa lugha ya kiingereza lina IF ya 1.4. Maandiko yanaweza kutumwa kwa mhariri kama anuani inavyooneshwa hapa chini:

Mchoro wa Stratigrafia ya Kimataifa

Tume ndogondogo za Kimataifa za IUGS zihusuzo Stratigrafia zinachangia kuboresha Mchoro wa Stratigrafia unaolenga kufafanua na kuhuisha Majina yatumikayo katika Stratigrafia ya Kimataifa. Toleo jipya linapatikana katika [www.stratigraphy.org](http://www.stratigraphy.org)

Anuani muhimu:

Sekretarieti ya IUGS

barua pepe: [secretariat@iugs.org](mailto:secretariat@iugs.org)

Dr Fareeduddin, Mhariri wa Matukio: barua pepe: [episodes.editor@gmail.com](mailto:episodes.editor@gmail.com)